# TAARIFA KWA UMMA

## KUWASILISHWA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA KWA MWAKA 2018

Leo tarehe 06 mwezi Novemba mwaka 2019 nimewasilisha mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Taarifa ya Hali Dawa za Kulevya ya Mwaka 2018. Taarifa hiyo imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 2017 kinachoielekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuiwasilisha bungeni kila mwaka Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini.

Lengo la Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ni kuwafahamisha wananchi hali ya tatizo la dawa za kulevya Nchini na jitihada zilizofanywa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo. Aidha, taarifa hii imewasilishwa kwa wabunge ili waweze kuwaelezea wananchi kwenye majimbo yao hali halisi ya tatizo la dawa za kulevya na jitihada zilizonywa na Serikali katika kudhibiti tatizo hilo.

Katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Mhe. Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli akifungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 20 Novemba, 2015 aliahidi kushughulikia mitandao ya wafanyabiashara wakubwa wanaojihusisha na dawa za kulevya bila ajizi. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 inasisitiza mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Katika kipindi cha mwaka 2018, vyombo vya dola kwa kushirikiana na wananchi viliendelea kutekeleza agizo la Rais na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 na kuiwezesha nchi yetu kupata mafanikio ambayo yalijidhihirisha kimataifa. Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), Tanzania ilipunguza uingizaji Nchini wa dawa ya kulevya aina ya heroin kwa asilimia 90.

Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali katika kupambana na dawa ya kulevya, bangi imeendelea kuwa tatizo kubwa hapa nchini. Mikoa ambayo imeonekana kuathirika zaidi na kilimo cha bangi ni pamoja na Mara, Tanga, Morogoro, Arusha, Kagera na Ruvuma. Pia, mirungi imeendelea kutumiwa na watu wa rika mbalimbali hapa Nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2018 juhudi za vyombo vya dola kwa kushirikiana na wananchi zilifanikisha ukamataji wa tani 24.3 za bangi zikiwahusisha watuhumiwa 10,061 na tani 8.97 za mirungi zikiwahusisha watuhumiwa 1,186.

Katika kipindi cha mwaka 2018 jumla ya kesi 7,593 zikiwa na jumla ya watuhumiwa 10,979 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Katika jumla ya kesi 7,174 zilizowahusisha watuhumiwa 11,045 ziliendelea kusikilizwa.

Serikali imeendelea kutoa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Jumla ya vituo sita vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Dodoma viliendelea kutoa huduma. Hadi kufikia mwaka 2018, zaidi ya watumiaji 8000 waliendelea kupatiwa huduma za Methadone katika vituo husika.

Serikali katika jitihada za kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ikiwemo taasisi za kimataifa, katika kuridhia na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa pia kuboresha sheria na kanuni za udhibiti dawa za kulevya pamoja na kutoa miongozo mbalimbali ambayo itaongeza tija na ufanisi katika kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya kwa mwaka 2018. Aidha, nachukua fursa hii pia kuwaomba wadau na wananchi kwa ujumla tuendelee kushirikiana katika kukabiliana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Jenista Joakim Mhagama (Mb)
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu**

(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu)